# Usalama wa Kiti cha Gari cha Mtoto

Kuanza Kwa Usalama

## Kinachoangalia Nyuma



Kwa watoto wachanga wenye umri wa hadi karibu miezi 30

## Kinachoangalia Mbele



Kiti hiki ni cha watoto ambao ni wakubwa kuzidi kiti chao kinachoangalia nyuma.

## Nyongeza



Kiti hiki humwinua mtoto ili mshipi wa kiti cha mtu mzima uweze kutoshea.

## Mshipi wa Kiti



Tumia jaribio la hatua 5 kuona ikiwa mtoto wako yuko tayari kutumia mshipi wa kiti.

Ni muhimu kwamba watoto **WASIHAMIE** kwenye kiti kinachofuata kabla ya kuwa tayari kwani hatua hii inaweza kusababisha jeraha kubwa. **Wakati wote tumia alama za bega kwenye kiti chako ili kukuongoza.**

Mikanda iko kwenye kiwango cha bega.

Angalia dhidi ya alama za urefu wa chini na juu, zilizoko kwenye kiti cha mtoto.

Hakikisha kwamba mikanda haijapinda na imeacha nafasi kidogo yenye upana wa kidole kinacholegea.



Hakikisha mkanda wa kufungia wa nyuma umewekwa kwenye sehemu sahihi ya kufungia.

Weka mtoto wako huku mgongo na makalio yakilalia kiti cha gari.

Hakikisha mshipi wa kiti umekazwa, ili kuweka kiti cha gari mahali pake.

Tafuta sehemu ya kufungia iliyowekwa kiwandani ya kiti cha mtoto (angalia mwongozo wa gari ikiwa huwezi kuipata) na uthibitishe kuwa unatumia sehemu sahihi ya kufungia ya gari lako.

Hakikisha mkanda wa juu wa kufungia umewekwa kwenye sehemu ya kufungia na umevutwa vizuri bila kulegea/nafasi na haujapinda

*Imewasilishwa na*

ROAD SAFETY EDUCATION VICTORIA

Starting Out Safely

EARLY LEARNING ASSOCIATION AUSTRALIA


VICTORIA State Government

# Usalama wa Kiti cha Gari cha Mtoto

Kwa viti vyote vya watoto vya gari na kapsuli, mkanda wa kufungia unapaswa kuwa umenyooka. Unaweza kuhitaji nyongeza ya mkanda wa kufungia ili kufikia sehemu ya kufungia.

Pia, iwapo kiti chako kina upau wa kuimarisha, hakikisha kwamba unautumia kiti kikiwa kimeelekezwa upande wa nyuma.


Tumia mshipi wa kiti au viuganisho vya Isofix.




Hakikisha unatumia sehemu sahihi ya kufungia ya kiti cha mtoto.

Tumia mwongozo wa gari lako kupata sehemu sahihi.

### Sehemu za kufungia




Hakikisha kiti kina Stika ya Kawaida Iliyoidhinishwa ya Australia na lebo inayoonyesha **AS/NZS 1754**. Stika **HAZIPASWI** kuwa zimeharibika au zimeondolewa. Viti visivyo na stika zinazofaa havipaswi kutumiwa.




Kabla ya kuhamisha mtoto kutoka Kiti cha Nyongeza cha Mtoto, **tafadhali hakikisha kwamba anakidhi hatua zote 5 za jaribio**.

Ikiwa hatapita hatua zote 5 lazima abaki kwenye Kiti cha Nyongeza.

Hii ni karibu sentimita 145

### JARIBIO LA HATUA TANO




1. Mgongo dhidi ya kiti cha gari
2. Magoti yanakunjika pembeni mwa kiti
3. Mshipi wa mapaja uko chini ukipita juu ya mapaja
4. Mshipi wa mabega unapita katikati ya bega
5. Anaweza kukaa katika mkao huu kwa muda wote wa safari

Mahali salama zaidi pa watoto kukaa ni kwenye viti vya nyuma. Watoto kuanzia umri wa miaka 12 walio na urefu wa zaidi ya sentimita 145 wanaweza kukaa kwenye kiti cha mbele.

Kamwe usiweke kiti cha gari kinachoangalia nyuma ambapo mfuko wa hewa unaotumika umewekwa.



Kwa maelezo zaidi nenda kwenye tovuti ya Kuanza kwa Usalama ya ELAA **www.childroadsafety.org.au**